



Ilikuwa Jumamosi asubuhi.
Maya, Dama na Dominic
walikuwa wakimsaidia
Mama Koki katika bustani
yake ya mboga. Watoto hao
walikuwa wakipalilia na
kunyunyizia mboga maji.
Baadaye, walichuma mboga
zilizokomaa. Kila mmoja
wao angepeleka nyumbani
stroberi, mchicha na karoti.




Mama Koki alipenda
kuwaandalia watoto
sherehe ndogo
walipomsaidia. Huwapatia
keki, chokoleti, au
peremende zinazofanana na
nyoka. Wakati mwingine
aliwapatia matofaa, pea au
machungwa. Mama Koki
alikuwa na sharti moja tu.
“Wagawe yote sawa!”
Watoto walijua kuwa ni
lazima wagawane kila kitu
walichopatiwa kwa kiasi
sawa.



Mama Koki alioka keki na watoto walisubiri kupatiwa ili wagawane. "Hii hapa keki!" Mama Koki alisema akitabasamu. "Kumbukeni sharti kwamba kila mmoja lazima apate kiasi sawa. Gaweni sawa! Mspigane!"



Maya alikuwa wa kwanza
kujaribu kugawa keki.
Alitumia kisu kuweka
mistari juu ya keki. Wengine
walimtazama. "Nitakata
sehemu tatu zilizo sawa!"
Maya alisema
akiwaonyesha.



"Hapana!" Dama alikataa.
"Kipande cha katikati ni
kikubwa zaidi!" Dominic pia
alitikisa kichwa. Maya
alicheka kisha akamwambia
Dama ajaribu kugawa.



"Nipe kisu nikate. Hii ni kazi rahisi!" Dama alisema. Kwanza alifuta mistari aliyoiweka Maya kisha akajlamba vidole.




Dama alianza kwa kugawa
kutoka juu hadi chini na
kutoka upande mmoja hadi
katikati. "Tazama, hizi ni
sehemu tatu!"

Maya na Dominic
walilalamika pamoja,
"Sehemu hizi tatu si sawa!"



"Gawanya sawa! Lazima kila
kipande kiwe na ukubwa
ulio sawa na umbo sawa,"
Dominic akaongeza.

Dama akajibu, "Dominic, si
ujaribu? Nina hakika
hutaweza!"



"Keki hii ingekuwa umbo la mraba au pembe nne, ingekuwa rahisi kugawa!"

Dominic alisema.

"Ingekuwa rahisi pia tungegawana tukiwa wanne." Maya aliongeza kusema.



Wakati huo, Dominic
alikumbuka gari la babake.
Lilikuwa na alama ya mistari
inayowezesha kugawa
sehemu tatu zilizo sawa.
Akasema, "Najua
tutakavyogawa."



Dominic akachora mistari
mitatu juu ya keki. Keki
ingekatwa kufuata mistari
hiyo, ingekuwa vipande
vitatu vilivyo sawa.




Dama alisema,
“Umetushangaza sana
Dominic. Umewezaje
kuhakikisha umegawa
vipande sawa?”

Dominic alitabasamu.
Hakutaka kuwaambia siri
yake.



Wakati huo, Mama Koki alitoka ndani ya nyumba akiwa amebeba bilauri za sharubati. "Mama Koki, Dominic amepata njia ya kukata keki vipande vitatu vilivyo sawa," Maya alimwambia.

"Hongera Dominic, umefaulu kugawa sehemu tatu zilizo sawa! Sasa ni wakati wa kwenda nyumbani," Mama Koki aliwaambia.



Kisha Maya alikata keki taratibu kufuata mistari iliyochorwa na Dominic. Watoto walihakikisha kwamba sehemu zote zilikuwa sawa. Kila mmoja akaiweka keki yake tayari kwenda nyumbani.



Babake Dominic alipowasili
kuwachukua watoto,
Dominic alimlaki akitaka
kumweleza jinsi alivyofaulu
kuigawa keki vipande vitatu
vilivyo sawa. Andika hapa
tafsiri ya maumbo haya.

